KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI KUSINI MASHARIKI YA ZIWA VICTORIA
SHULE YA SEKONDARI YA MWADUI
S.L.P. 51,
MWADUI.

SIMU: NO.0754 – 071178/0766-179519
Email:mwadui. Lutheran. sec.@Email.com

1. School Vision: " Providing Education Capable of Developing Human Potentials"
2. School Mission: "To promote and Develop Quality Education Capable for promoting Human Potentials"
3. School Motto: "Success Through Co-operation"

MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA MWADUI SEKONDARI 2017
(JOINING INSTRUCTIONS 2017)

Ndugu ……..
S.L.P. ……..
……

1.0 **UTANGULIZI:**
Bwana Mungu wetu na apewe Sifa,

Ninayo furaha kukujulisha kuwa maombi yako ya kujiunga na Shule ya Mwadui Sekondari **Kidato cha …… Mwaka ……** yamekubaliwa. Shule itafunguliwa Tarehe ……

"HONGERA SANA"

Shule hii ipo ndani ya Mgodi ya Williamson Diamonds Ltd. Mwadui ina mazingira mazuri ya kumuwezesha mwanafunzi kusoma na kufaulu vizuri mitihani yake. Shule hii inamilikiwa na **KANISA LA KILUTHERI TANZANIA – DAYOSISI KUSINI MASHARIKI YA ZIWA VICTORIA**. Tunapokea wanafunzi wa **IMANI** zote ili mradi aoneshe **NIDHAMU, UTII, BIDII YA MASOMO** na **MAADILI MEMA**. Somo la MAADILI (Moral Life and Human Ethis) linapewa kipaumbele kwa muda wote. Pia shule imeanzisha kidato cha **TANO** na **SITA** na usajili toka **W**izarani umeshakamilika na masomo yameshaanza tayari kwa Tahasusi (combination zifuatazo **PCM, PCB, CBG, HKL, HGL na HGK** nafasi bado zipo unakaribishwa.

2.0 **SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

1. Shule inazo sheria ambazo kila mwanafunzi atapewa na anatakiwa kuzifuata. Kuvunja sheria za shule ni sawa na kuvunja mkataba na shule. Hivyo, mwanafunzi akivunja sheria za shule anaweza kuadhibiwa au kusimamishwa au kufukuzwa shule.

2. Mwanafunzi anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa kuwa Kiongozi wa wanafunzi wenzake. Hatakiwi kukataa wadhifa atakaopewa. Akiwa katika wadhifa huo ataongoza wanafunzi wenzake kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria za shule bila upendeleo wowote.

3. Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki ipasavyo katika michezo kwani michezo ni Afya mwanafunzi aje na nguo za michezo.

4. Mwanafunzi anatakiwa aoneshe nidhamu ya hali ya juu wakati wote na kwa watu wote. Pia anatakiwa kuonesha ushirikiano katika kukamilisha majukumu mbalimbali (participatory works).

5. Kila mwanafunzi atatakiwa kufanya mitihani yote itakayotolewa shuleni (weekly Test, Monthly Test, na Joint Exams) bila kukosa hata mmoja kutofanya hivyo mwanafunzi atarudishwa nyumbani.

- Wakati wote anatakiwa kutumia lugha ya heshima kama vile “Thank you” “Excuse me” “I am sorry” “Please forgive me”.

- Mwanafunzi anatakiwa kuonesha utayari wa kusahihishwa na kuonesha nidhamu anapodai haki zake.

6. Wageni wote wa wanafunzi wanatakiwa kuandikishwa katika kitabu cha wageni wa wanafunzi kila mgeni wa mwanafunzi ambaye ameandikwa kwenye fomu No.2 katika kipengele cha 5 (i) – (iii) ndiye atakayetambuliwa na uongozi wa shule na ni lazima kwanza aonane na uongozi wa shule/mwalimu wa zamu kabla ya kuonana na mwenyeji wake (mwanafunzi).

3.0 **AMRI ZA MUNGU**

Ni sharti mwanafunzi aoneshe utii mbele za Mungu na watu wote. Hivyo basi awe Mcha Mungu asiwe na tamaa ya vitu asizini, asiue wenzie kwa kuwakatisha tamaa katika kufanikisha malengo yao bali awatie moyo.

4.0 **SOMO LA BIBLIA (BIBLE KNOWLEDGE)**

Kila mwanafunzi anapaswa kusoma somo la Bible Knowledge bila kujali itikadi za dini na kuhakikisha amefanya mitihani yake yote. Kutakuwa na ibada moja tu ya shule, kila siku asubuhi na jioni pia kwa utaratibu wa kanisa.

5.0 **SHERIA YA KUZUNGUMZA KIINGEREZA (ENGLISH SPEAKING RULE)**

Lugha rasmi shuleni ni Kiingereza peke yake, isipokuwa katika kipindi cha somo la Kiswahili tu. Hivyo kila mwanafunzi ajitahidi na kujibidiisha katika kujifunza lugha hiyo.

ADA:

1. Ada ya Shule ni	Tshs.1,500,000/=(Bweni)
	Tshs. 1,250,000/= (Day)
2. Sweta 1	Tshs.15,000/=
3. Tshirt 2 @ 10,000	Tshs.20,000/=
4. Usajili na kitambulisho	Tshs.30,000/=
5. Ukaguzi/OHONGSS/TOMONGS/INSENT/UMISSETA..	Tshs.20,000/=
6. Kompyuta/.....	Tshs.100,000/=
7. Maabara	Tshs. 20,000/=
8. Matibabu ya huduma ya kwanza shuleni	Tshs.30,000/=

- **Mwanafunzi akitibiwa nje ya shule Mzazi atalipia Gharama hizo.**

NB: ADA ITALIPWA KWA AWAMU

Awamu Tatu ni kama ifuatavyo:

(a) Tshs.500,000/=
(b) Tshs.500,000/=
(c) Tshs.500,000/=

Awamu mbili

(a) Tshs.750,000/=
(b) Tshs.750,000/=

Awamu Moja

(a) 1,500,000/=

5. Michango mingine kama Mitihani ya NECTA, MOCK, JOINT italipwa na mwanafunzi kadiri inavyohitajika

SARE ZA SHULE
WASICHANA

1. Sketi mbili (2) **Nyeusi** au zaidi mshono wenye marinda ya kawaida ya kuzunguka sketi isiwe Linda box au solo ziwe ndefu zinazovuka magoti **kwa urefu wa nchi kumi na Tano** kitambaa cha suti aje nazo.
2. Sweta na Tshirt zinapatikana shuleni atazilipia kama inavyoonekana kwenye kipengele cha ADA No.2 & 3.
3. Shati mbili nyeupe au zaidi zenye mikono mifupi na za kusitili mwili wake vizuri aje nazo.

WAVULANA

1. Suruali mbili (2) **Nyeusi** za kitambaa cha shuti au zaidi zenye upana wa sentimeta 16 cm kwenye upana wa miguuni aje nazo.
2. Sweta na Tshirt zinapatikana shuleni atazilipia kama inavyoonekana kwenye kipengele cha ADA No.2 & 3.
3. Shati mbili nyeupe au zaidi zenye mikono mifupi na za kusitiri mwili wake vizuri aje nazo.

Mzazi/Mlezi unashauriwa kulipia mahitaji yote ya shule kwa kupitia Benki ya NMB (National Microfinance Bank) iliyo karibu na wewe:

AKAUNTI YA SHULENI NI: MWADUI SEKONDARI
NMB MWADUI BRANCH A/c 32406600003

MALIPO YOYOTE YALE YAKISHAKATIWA STAKABADHI YA SHULE HAYARUDISHWI

6.0 **UVAAJI WA SARE ZA SHULE**

Sare ya shule itavaliwa na mwanafunzi anapotoka nyumbani kwao kuja shuleni, anapotoka likizo kurudi shuleni, anaporudi nyumbani kwao wakati wa likizo pamoja na kipindi chote awapo shuleni isipokuwa pale tu itakapoelezwa tofauti. Kwa wasichana sketi zote zinatakiwa ***kuvuka magoti kwa urefu wa nchi kumi na Tano.*** Na kwa wavulana ni marufuku kuvaa ***mtepesho*** na kutochomekea mashati pia suruali za kubana (modo) hazitakiwi.

7.0 **VIFAA NA MAHITAJI MENGINE**

Kwa wanafunzi wanaoanza **Kidato cha kwanza** na wale wahamiaji wanatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo siku anaporipoti shule.

1. **Form one :** anatakiwa kuja na **Ream mbili (2) A4** fyekeo, jembe na mpini wake
2. **Wanaohamia:** anatakiwa aje na **Ream mbili (2) A4** Rake moja na mpini wake

Na kila mwanafunzi atafanyiwa ukaguzi wa vitu vyote alivyokuja navyo na pia kuhakikisha kama atakuwa amekidhi mahitaji yote ya shule anayotakiwa kuja nayo shuleni.

A. MAHITAJI MENGINE MUHIMU ANAYOTAKIWA KUWA NAYO MWANAO NI:

S/N	KIFAA	IDADI
1.	Biblia ya Kiswahili 1	1
2.	Shati nyeupe za mikono mifupi mbili zisiwe za kubana	2
3.	Viatu vya ngozi rangi nyeusi, sori fupi pair mbili zenye kamba	2
4.	Socks nyeupe pair tatu (3) au zaidi	3
5.	Raba za michezo pair moja	1
6.	Bukta za michezo na Track suit ndefu) pair 1	1
7.	Madaftari makubwa (counter Books – quires 3)	15
8.	Rula 30 cm	1
9.	Spring files	2
10.	Rimu mbili za karatasi (A4)	2
11.	Picha Passport size	4
12.	Mfagio mrefu wa nje mmoja wa kukwaruza	1
13.	English Advanced Learners Dictionary	1
14.	School Bag (Begi la shule)	1
15.	Sahani kikombe na kijiko kwa ajili ya kulia chakula	1

B:MAHITAJI MENGINE WANAYOTAKIWA KUWA NAYO WANAFUNZI WA BWENI

S/N	KIFAA	IDADI
1.	Godoro (2 x 2 ½)	1
2.	Mashuka rangi ya Pinki mawili	2
3.	Chandarua kimoja kinacholingana na godoro	1
4.	Ndoo	1
5.	Mto na foronya	1
6.	Nguo za michezo kwa jinsia na nguo za ndani za kutosha	
7.	Taulo na mahitaji yote yanayohusu kuoga, kufua na afya katika mazingira ya bweni	
8.	Sanduku imara la kutunza vifaa vyake (Tranka)	1
9.	Kwa tahadhari ni vyema kuja na Tochi (kurunzi)	1

B. **MAMBO YASIYOTAKIWA KABISA SHULENI WAKATI WOTE**

1. Uzembe wa aina yoyote ile darasani au nje ya darasa hautakiwi.
   Mwanafunzi ataendelea na darasa baada ya kufikisha au kuvuka wastani uliowekwa na Bodi ya Shule ambao ni alama 41.
2. Ni marufuku kuonesha au kujaribu kuonesha mahusiano ya kimapenzi
   Wanafunzi wote waheshimiane na kuishi maisha ya familia moja kama Dada na Kaka.
3. Nguo ambazo siyo sare ya shule ni marufuku kuonekana katika mazingira ya shule.
4. Huruhusiwi kuvaa viatu ambavyo siyo sare ya shule
5. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja na simu shuleni au laini ya simu Mwanafunzi atakayekaidi agizo hili na akakamatwa na simu atataifishwa simu hiyo bila masharti yoyote na yeye kufukuzwa shule.
6. Mwanafunzi hatakiwi kudharau viongozi wake (viranja/viongozi wa dini/walimu na wafanyakazi wa shule.
7. Mwanafunzi unatakiwa kuzitii sheria, kanuni na taratibu zote utakazoelekezwa ukiwa shuleni.
8. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha ndefu, ndevu,kupaka rangi,kuvaa bangili, hereni, mkufu, kufunga kitambaa kichwani na kunyoa kipara au kunyoa panki hairuhusiwi.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na chakula cha aina yoyote kutoka nyumbani anaporudi shuleni kutoka likizo.

“MKAMATE ELIMU, USIMWACHE, AENDE ZAKE MSHIKE, MAANA YEYE NI UZIMA WAKO” (Mithali 4:13)

“KARIBU SANA

MKUU WA SHULE

KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI KUSINI MASHARIKI YA ZIWA VICTORIA
SHULE YA SEKONDARI YA MWADUI

S.L.P. 51,
MWADUI.

SIMU: No.0754-071178/0766179519
Email:mwaseco2008@yahoo.com

FOMU NO.1

FOMU MAALUMU KWA MWANAFUNZI ANAYEJIUNGA

1. Jina la Mwanafunzi
   .....Jinsia: (Ke/Me)
2. Mwaka aliomaliza Darasa la saba .....
3. Shule aliyomalizia .....
4. Namba yake ya Mtihani ..... Wilaya ya.....
5. Mkoa wa .....

1. .....
JINA NA SAHIHI YA MKUU WA SHULE ALIPOMALIZA KIDATO CHA NNE

KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI KUSINI MASHARIKI YA ZIWA VICTORIA
SHULE YA SEKONDARI YA MWADUI
S.L.P. 51,
MWADUI.
SIMU: No.0754-071178./0766179519
Email:mwaseco2008@yahoo.com

FOMU NO.2
KUKUBALIANA NA MASHARTI YA SHULE

1. Mimi (mwanafunzi)

   .....

   Ninayeomba nafasi ya masomo Kidato cha .....
   Ninaahidi kutii na kutekeleza masharti na maelekezo mbalimbali ya shule chini ya uongozi wa shule ikiwa ni pamoja na mipango ya kiutendaji kitaaluma itakayokuwa inaandaliwa na uongozi wa shule.
2. Kama mwanafunzi wa HOSTEL naahidi kuwa mtii na mnyenyekevu mahali pote na nyakati zote pamoja na kuzitii kanuni zote za HOSTEL.
3. Mimi ..... Nikiwa shuleni nitahudhuria vipindi vya dini (Bible knowledge) na kufuata kanuni zote za HOSTEL.
4. Nikikiuka sheria, kanuni na taratibu za shule nipo tayari kuadhibiwa kadri ninavyostahili.
5. Andika majina ya watu watatu ambao watatambuliwa na uongozi wa shule kwa mawasiliano.

(a) **LAZIMA AWE MZAZI AU MLEZI.....**

S.L.P. ..... SIMU NO. ...../ .....

(b) **LAZIMA AWE NDUGU WA KARIBU (DADA AU KAKA).....**

S.L.P. ..... SIMU NO:...../.....

(C) **YEYOTE ANAYETAMBULIWA NA MZAZI/MLEZI.....**

S.L.P..... SIMU NO ...../.....

.....
JINA LA MWANAFUNZI NA SAHIHI YAKE